

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI.

SHULE YA SEKONDARI JAILA,
S. L. P 77,
PSONGE – KILINDI
SIMU: 0629 699773

Tarehe

Kumb. Na. JSS/RGE/VOL 01/.....

Ndugu,

S. L. P

.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA

1. UTANGULIZI.

Mpendwa mwanafunzi,

Nakupa pongezi nyingi kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na shule hii. Nafasi uliyoipata ni adimu sana, na kwamba wengi walikuwa wanaipigania kwa UDI na UVUMBA, lakini hawajaipata. Kwa hali hiyo sharti uitumie nafasi hii vizuri kadri ya uwezo wote ili mwishowe upate elimu bora itakayokuletea manufaa wewe binafsi, wazazi wako na Taifa kwa ujumla.

Walimu, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wote kwa pamoja huunda jumuiya ya shule inayotegemeana, inakuwa ni familia moja yenye lengo moja la kutekeleza sera ya ELIMU. Hivyo kila ajiungaye na shule hii ni lazima awe tayari KUJIFUNZA, KUJITUMA na KUJITEGEMEA.

Jumuiya ya shule hii inakukaribisha na kukutakia safari njema wakati wa kuja.

2. KUFUNGUA.

Shule itafunguliwa tarehe 04/1/2021 Unatakiwa uwepo shuleni saa 1:30 asubuhi, ukiwa na mahitaji yote ya shule kama itakavyo elekezwa hapo chini. Mwanafunzi atakayechelewa au kufika bila mahitaji aliyoagizwa hatavumiliwa.

3. MAHITAJI YA SHULE.
SARE YA SHULE.

Mwanafunzi anatakiwa awe anavaa sare ya shule wakati wote anapokuwa shuleni. Hivyo uje na sare inayokuhusu kijinsia na zingatia rangi na mshono ulioelekezwa, lasivyo utalazimika kushona sare nyingine.

A. WASICHANA

- i. Sketi (skirt) mbili ndefu, rangi ya udhurungi. Sketi iwe na marinda sita.
- ii. Shati / blauzi mbili nyeupe, ziwe za mikono mifupi.
- iii. Skafu rangi ya udhurungi
- iv. Viatu vyeusi vinavyofunika miguu na viwe vya kamba na soksi nyeupe jozi mbili
- v. Hijabu nyeupe ndefu.
- vi. Rangi ya sweta utaikuta shuleni.

B. WAVULANA

- i. Suruali mbili rangi ya udhurungi zenye marinda.
- ii. Shati mbili nyeupe, ziwe za mikono mifupi.
- iii. Tai ndefu ya rangi ya udhurungi
- iv. Viatu vyeusi vinavyofunika miguu na viwe vya kamba na soksi nyeusi jozi mbili.
- v. Rangi ya sweta utaikuta shuleni.

ZINGATIA: kitambaa cha rangi ya suruali, tai, sketi na skafu kimeambatanishwa.

4. MAHITAJI MENGINE.

Kila mwanafunzi anapaswa kuja na mahitaji yafuatayo:-

- i. Daftari (counter books) kumi na mbili (12), rula, kalamu, penseli na mkebe (mathematical set)
- ii. Kamusi ya Kiswahili moja (1) na English Dictionary moja (1)
- iii. Begi zuri la shule.
- iv. Ufagio wa chelewa 1
- v. Jembe na mpini wake kwa wasichana, wavulana kwanja na panga.

5. MAHITAJI YA CHAKULA.

Chakula cha mchana shuleni ni cha lazima na kila mwanafunzi aje na mahitaji yafuatayo:-

- i. Sembe kilo 4 kwa kila mwezi
- ii. Maharage kilo 2 kwa kila mwezi
- iii. Shilingi 2,000/= kwa ajili ya mpishi na viungo kwa kila mwezi.

MUHIMU: Mahitaji yote ya chakula mwanafunzi anapaswa kuja nayo siku anayoripoti shule.

6. FOMU ZA KUKAMILISHA NA KUJA NAZO.

Fomu ya kupimwa Hospitalini (Medical Examination Form). Hati hii ijazwe na Daktari/ Mganga wa Hospitali ya Mkoa/Wilaya au kituo cha Afya (siyo Zahanati) ambaye atakupima kadri ya maelekezo ya fomu hii.

Ni muhimu umfahamishe Mganga matatizo yoyote ya kiafya uliyonayo ili itusaidie sisi jinsi ya kukuhudumia pindi uwapo shuleni.

7. MWISHO.

Ndugu mwanafunzi, tunakutegemea kuwa, kwa wakati wote unapokuwa hapa, utakuwa MWADILIFU na mwenye NIDHAMU ya hali ya juu. Taifa limekupatia DHAMANA hii ili hatimaye utoe matunda yenye manufaa kwa TAIFA, JAMII YAKO na WEWE BINAFSI. Hivyo utatakiwa kuthibitisha kuwa HALI na VITENDO kuwa hutachezea nafasi hii adimu. Itakuwa ni kosa kubwa kuwa msaliti wa dhamana hii kwa kutenda kinyume cha taratibu za shule na Elimu kwa ujumla.

KARIBU SANA SEKONDARI YA JAILA.



.....
S. S. KAPATE

**MKUU WA SHULE.
THE HEADMASTER
JAILA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 77 SONGBE
DATE.....**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF LOCAL AND REGIONAL GOVERNMENT ADMINISTRATION**

JAILA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 77,
SONGE – KILINDI

DATE:

**THE MEDICAL OFFICER,
P. O. BOX**

Dear Sir/Madam,

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine Mr./Miss as to his / her fitness as a full time student of this school.

May I kindly ask you to fill in the particulars given in the form here under

Yours sincerely,

.....
THE HEADMASTER

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a Medical Officer in respect of all form I entrants.

Pupil's Full name

Age and Sex

Blood found (red and White)

Stool Examinations

Urine analysis

Syphilis and other

General Diseases test

T.B Test

Eye test

Ears

Chest

Spleen

Abdomen

Urine for planet

Additional information (If any e.g. Physical defects important (s) (e.g. arm leg etc) infections

chronic or family diseases etc

.....

.....

.....

.....

.....

I certify that the above is fit/unfit to pursue further execution on as stated above.

Signature

Designation

Station

Date